## 22- Wasiojaaliwa Kwenda Kutekeleza Hajj

Waislamu wasiojaaliwa kwenda kutekeleza Hajj watambue kwamba nao wana fursa ya kujichumia thawabu tele kwa kutekeleza 'ibaadah zenye fadhila tukufu kuanzia tarehe 1 Dhul-Hijjah mpaka tarehe 13 Dhul-Hijjah kama Alivyotuamrisha Allaah (سبحانه وتعالى) na Rasuli Wake (صلى الله عليه وآله وسلم).

### 1 - Allaah Ameziapia Siku Kumi Hizi

Kwa jinsi zilivyokuwa na umuhimu mkubwa siku hizo kumi, hadi kwamba Allaah (سبحانه وتعالى) Ameziapia katika Qur-aan Anaposema:

﴿ وَٱلۡفَجۡرِ ۝١ وَلَيَالٍ عَشۡرٍ ۝٢ ﴾

**((Naapa kwa Alfajiri. Na (kwa) masiku kumi))**[1]

Wanachuoni wafasiri wa Qur-aan wamekubaliana kwamba zilizokusudiwa hapo ni Siku kumi za Dhul-Hijjah.

### 2 - 'Amali Zake Ni Bora Kuliko Kwenda Katika Jihaad Fiy SabiyliLLaah

Kutokana na ilivyotajwa katika usimulizi wa Hadiyth ifuatayo, kwamba 'amali yoyote utendayo katika masiku kumi hayo, ni bora kuliko kwenda kupigana jihaad vitani. Ukizingatia kwenda kupigana jihaad ni jambo zito mtu kuliitikia, kwani huko kuna mashaka mbali mbali, ikiwemo khofu ya kujeruhiwa na kupoteza viungo vya mwili, kufariki, kupoteza mali n.k. Ila hilo si zito kwa mwenye iymaan ya hali ya juu kabisa kutaka kuyakabili mashaka hayo na kutamani kufa shahidi. Kwa hiyo usidharau 'amali yoyote hata iwe ndogo vipi itekeleze kwani Allaah (سبحانه وتعالى) ni *Al-Jawwaad* (Mwingi wa ukarimu), *Al-Kariym* (Mkarimu), *Al-Wahhaab* (Mwingi wa kutunuku, Mpaji wa yote), *Al-Majiyd* (Mwingi mno wa vipawa na ukarimu).

[1] Al-Fajr (89: 1-2).

Hadiyth ya Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) kwamba Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema:

**((مَا مِنْ أَيَّامٍ الْعَمَلُ الصَّالِحُ فِيهَا أَحَبُّ إِلَى اللَّهِ مِنْ هَذِهِ الْأَيَّامِ)) يَعْنِي أَيَّامَ الْعَشْرِ. قَالُوا: يَا رَسُولَ اللَّهِ: وَلَا الْجِهَادُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ؟ قَالَ: ((وَلَا الْجِهَادُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ إِلَّا رَجُلٌ خَرَجَ بِنَفْسِهِ وَمَالِهِ فَلَمْ يَرْجِعْ مِنْ ذَلِكَ بِشَيْءٍ))**

***((Hakuna siku ambazo vitendo vyake vyema Anavipenda Allaah kama siku kumi hizi)) yaani siku kumi za mwanzo wa mwezi wa Dhul-Hijjah)).*** Akaulizwa, je, hata jihaad katika njia ya Allaah? Akasema: ***((Hata jihaad katika njia ya Allaah isipokuwa mtu aliyekwenda na nafsi yake na mali yake ikawa hakurudi na kimojawapo))***[2]

### 3 - Siku Za Manufaa Na Kumkumbuka Allaah

Inapasa kumdhukuru mno Allaah (سبحانه وتعالى) kwa kukumbuka Neema Zake zisizohesabika:

﴿ لِّيَشْهَدُواْ مَنَـٰفِعَ لَهُمْ وَيَذْكُرُواْ ٱسْمَ ٱللَّهِ فِىٓ أَيَّامٍ مَّعْلُومَـٰتٍ ﴾

**((Ili washuhudie manufaa yao; na walitaje Jina la Allaah katika siku maalumu))**[3]

Ibn 'Abbaas kasema: "Hizo ni siku kumi za Dhul-Hijjah." Na Amesema: "Manufaa ya dunia hii na ya Aakhirah." Manufaa ya Aakhirah yanajumuisha kupata Radhi za Allaah. Manufaa ya vitu vya dunia inajumuisha wanyama wa kuchinjwa na biashara.[4]

### 4 - 'Ibaadah Zote Zimejumuika Katika Siku Hizi

'Ibaadah zote zimejumuika katika siku kumi hizi nazo ni Swalaah, Swawm, Swadaqah na Hajj; wala hazijumuiki hizi katika wakati mwengine.

---

[2] Al-Bukhaariy, Abu Daawuwd, Ahmad, Ibn Maajah.
[3] Al-Hajj (22: 28).
[4] Tafsiyr Ibn Kathiyr.

## 5 - ’Amali Njema Za Kufanya Katika Siku Kumi Hizi

### i- Kuomba Tawbah ya kweli na kujiepusha na maasi:

Muislamu anapaswa kila siku kuomba tawbah kwa Allaah (سبحانه وتعالى). Juu ya kuwa Allaah (سبحانه وتعالى) Anamghufuria madhambi mja Wake, tawbah pia ina faida kadhaa tukufu kama zilivyotajwa katika Qur-aan na Sunnah. Kwa hiyo, masiku haya usikose kujizidishia fadhila zake. Allaah (سبحانه وتعالى) Ameamrisha mpaka Waumini kuomba tawbah:

﴿ وَتُوبُوٓاْ إِلَى ٱللَّهِ جَمِيعًا أَيُّهَ ٱلۡمُؤۡمِنُونَ لَعَلَّكُمۡ تُفۡلِحُونَ ﴿٣١﴾ ﴾

**((Na tubuni kwa Allaah nyote, enyi Waumini mpate kufaulu))**[5]

### ii- Kumdhukuru sana Allaah (سبحانه وتعالى):

Inapasa kumdhukuru mno Allaah (سبحانه وتعالى) kwa *Tasbiyh, Tahmiyd, Tahliyl, Takbiyr* (kusema: Subhaana Allaah, AlhamduliLlaah, Laa Ilaaha Illa Allaah, Allaahu Akbar).

عن ابْنِ عُمَرَ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَال: **((مَا مِنْ أَيَّامٍ أَعْظَمُ عِنْدَ اللَّهِ وَلَا أَحَبُّ إِلَيْهِ مِنَ الْعَمَلِ فِيهِنَّ مِنْ هَذِهِ الْأَيَّامِ الْعَشْرِ فَأَكْثِرُوا فِيهِنَّ مِنَ التَّهْلِيلِ وَالتَّكْبِيرِ وَ التَّحْمِيدِ))** أخرجه أحمد

Imepokelewa toka kwa Ibn 'Umar (رضي الله عنهما) kwamba Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***((Hakuna siku zilizokuwa tukufu kwa Allaah na zilizokuwa vitendo vyake vipenzi kabisa Kwake kama siku hizi, basi zidisheni Tahliyl na Takbiyr na Tahmiyd))***[6]

Inavyopasa kufanya takbiyr:

**الله أكبر. الله أكبر. لا إله إلا الله. والله أكبر. الله أكبر ولله الحمد**

---

[5] An-Nuwr (24: 31).

[6] Ahmad.

***"Allaahu Akbar, Allaahu Akbar, Laa Ilaaha Illa Allaah Wa-Allaahu Akbar, Allaahu Akbar WaliLLaahil-Hamd"***

"Allaah ni Mkubwa, Allaah ni Mkubwa, hapana ilaah (muabudiwa wa haki) isipokuwa Allaah, na Allaah ni Mkubwa, Allaah ni Mkubwa, na kuhimidiwa ni kwa Allaah (Pekee)

Takbiyr hii ni aina mbili:

***Takbiyr Al-Mutwlaq***: Za Nyakati Zote: Takbiyr wakati wote usiku au mchana tokea unapoingia mwezi wa Dhul-Hijjah na inaendelea mpaka siku ya mwisho ya *Tashriyq* (tarehe 13 Dhul-Hijjah) baada ya magharibi. Inaletwa mahali popote; sokoni, njiani, majumbani n.k.

***Takbiyr Al-Muqayyad***: Za Nyakati Maalumu: Takbiyr baada ya kila Swalaah na huanza baada ya Swalaah ya Alfajiri siku ya '*Arafah* mpaka baada ya Swalaah ya Alasiri ya tarehe 13 Dhul-Hijjah.

**iii- Kufufua Sunnah ya Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم):**

Wanaume wanatakiwa waseme kwa sauti ili kuwakumbusha wengine na kufufua Sunnah ya Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) na wanawake waseme kimya kimya isipokuwa wakiwa na mahaarim wao. Kufufua Sunnah ya Nabiy ni muhimu kwani bila ya kufanya hivyo tutakuwa kwanza tunakosa fadhila zake, pili zitapotea Sunnah za kiongozi wetu Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم):

**كَانَ ابْنُ عُمَرَ وَأَبُو هُرَيْرَةَ يَخْرُجَانِ إِلَى السُّوقِ فِي أَيَّامِ الْعَشْرِ يُكَبِّرَانِ وَيُكَبِّرُ النَّاسُ بِتَكْبِيرِهِمَا**

"Ibn 'Umar na Abu Hurayrah walikuwa wakienda sokoni katika siku kumi na kufanya Takbiyr kwa sauti na watu wakiwaigiza."[7]

**iv- Kuzidisha 'amali njema mbali mbali:**

---

[7] Al-Bukhaariy.

Kutekeleza fardhi ya Swalaah kwa kuswali kwa wakati wake, kuswali Sunnah zaidi, kusoma Qur-aan, swadaqah, du'aa, kutii wazazi na kuwafanyia wema, kuwasiliana na jamaa (kuunga undugu), kuwafanyia wema jirani, kuamrishana mema na kukatazana maovu, kufanyiana wema na ihsani na kila aina ya jema hata dogo vipi, kwani huenda likawa ni lenye kumridhisha Allaah (سبحانه وتعالى) mno.

**v- Kufunga siku hizi khaswa siku ya *'Arafah*[8]:**

عَنْ أَبِي قَتَادَةَ رضي الله عنه أن النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: ((**صِيَامُ يَوْمِ عَرَفَةَ أَحْتَسِبُ عَلَى اللَّهِ أَنْ يُكَفِّرَ السَّنَةَ الَّتِي قَبْلَهُ وَالسَّنَةَ الَّتِي بَعْدَهُ**)) أخرجه مسلم

Imepokelewa toka kwa Abu Qataadah (رضي الله عنه) ambaye amesema: Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) kasema kuhusu Swawm ya '*Arafah* kuwa ***((inafuta madhambi ya mwaka uliopita na wa baada yake))***[9]

**vi- Kuchinja baada ya Swalaah ya 'Iyd:**

'Ibaadah tukufu na ni Sunnah iliyosisitizwa na Wanachuoni wameona kuwa ni waajib kwa kila aliyekuwa na uwezo kwake kuchinja. Anasema Allaah (سبحانه وتعالى):

﴿ فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَٱنْحَرْ ۝٢ ﴾

**((Basi Swali kwa ajili ya Rabb wako na uchinje))[10]**

فعَنْ أَنَسٍ رضي الله عنه قَالَ: ((**ضَحَّى النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بِكَبْشَيْنِ أَمْلَحَيْنِ أَقْرَنَيْنِ ذَبَحَهُمَا بِيَدِهِ وَسَمَّى وَكَبَّرَ وَوَضَعَ رِجْلَهُ عَلَى صِفَاحِهِمَا**)) متفق عليه

[8] Rejea Mlango wa "Historia Fupi Ya Makkah Na Kuhusu Hajj Na 'Umrah."
[9] Muslim.
[10] Al-Kawthar (108- 2).

Imepokelewa toka kwa Anas (رضي الله عنه) kwamba Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) alichinja kondoo wawili weupe[11] wenye pembe, amewachinja kwa mikono yake, akasema *BismiLLaah* na *Allaahu Akbar* na akaweka mguu wake upande wa nyuma yao."[12]

Kuchinja kuna hikmah kubwa ndani yake na fadhila zake ni adhimu. Anasema Allaah (سبحانه وتعالى):

﴿ لَن يَنَالَ ٱللَّهَ لُحُومُهَا وَلَا دِمَآؤُهَا وَلَٰكِن يَنَالُهُ ٱلتَّقْوَىٰ مِنكُمْ ۚ كَذَٰلِكَ سَخَّرَهَا لَكُمْ لِتُكَبِّرُوا۟ ٱللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَىٰكُمْ ۗ وَبَشِّرِ ٱلْمُحْسِنِينَ ﴿٣٧﴾ ﴾

**((Haimfikii Allaah nyama zake wala damu yake, lakini inamfikia taqwa kutoka kwenu. Hivyo ndivyo Tulivyowatiisha (hao wanyama) kwenu ili mpate kumtukuza Allaah (kusema: *Allaahu Akbar*) kwa yale Aliyokuongozeni; na wabashirie wafanyao ihsaan.))**[13]

عَنْ عَائِشَةَ (رضي الله عنها) أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: **((مَا عَمِلَ آدَمِيٌّ مِنْ عَمَلٍ يَوْمَ النَّحْرِ أَحَبَّ إِلَى اللَّهِ مِنْ إِهْرَاقِ الدَّمِ, إِنَّهَا لَتَأْتِي يَوْمَ الْقِيَامَةِ بِقُرُونِهَا, وَأَشْعَارِهَا, وَأَظْلَافِهَا وَأَنَّ الدَّمَ لَيَقَعُ مِنْ اللَّهِ بِمَكَانٍ قَبْلَ أَنْ يَقَعَ مِنْ الْأَرْضِ فَطِيبُوا بِهَا نَفْسًا))**

Imepokelewa toka kwa 'Aaishah (رضي الله عنها) kwamba Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***((Hakuna kitendo cha bin Aadam kilichokuwa ni kipenzi kabisa kwa Allaah siku ya kuchinja kama kumwaga damu. Atakuja (huyo mnyama) siku ya Qiyaamah na pembe zake, kucha zake na nywele zake. Damu yake itamwagika mahali fulani Allaah Anapajua kabla ya kumwagika katika ardhi. Hivyo zipendezesheni nafsi kwayo))***[14]

Na Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) alipoulizwa:

---

[11] Baadhi ya wanachuoni wamesema kuwa ni weupe ulio na alama nyeusi, wengine wamesema uliochanganyika na wekundu.
[12] Al-Bukhaariy na Muslim.
[13] Al-Hajj (22: 37).
[14] At-Tirmidhiy, Sunan Ibn Maajah.

مَا هَذِهِ الْأَضَاحِيُّ؟ قَالَ: ((**سُنَّةُ أَبِيكُمْ إِبْرَاهِيمَ**)) قَالُوا: فَمَا لَنَا فِيهَا يَا رَسُولَ اللَّهِ؟ قَالَ: ((**بِكُلِّ شَعَرَةٍ حَسَنَةٌ**)) قَالُوا: فَالصُّوفُ يَا رَسُولَ اللَّهِ؟ قَالَ: ((**بِكُلِّ شَعَرَةٍ مِنْ الصُّوفِ حَسَنَةٌ**))

"Nini hivi vichinjo?" Akajibu: ***((Ni Sunnah ya baba yenu Ibraahiym)).*** Wakasema, "Nini umuhimu wake kwetu?" Akasema: ***((Katika kila unywele kuna jema moja))*** Wakasema: "Na sufi?" Akasema: ***((Katika kila unywele wa sufi kuna jema moja))***[15]

**Yanayompasa Kufanya Mwenye Kutaka Kuchinja**

Baada ya kutia niyyah ya kuchinja, asikate mtu nywele wala kucha mpaka 'amalize kuchinja kama tulivyoamrishwa katika Hadiyth ifuatayo:

عَنْ أُمِّ سَلَمَةَ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: ((**إِذَا رَأَيْتُمْ هِلَالَ ذِي الْحِجَّةِ وَأَرَادَ أَحَدُكُمْ أَنْ يُضَحِّيَ فَلْيُمْسِكْ عَنْ شَعْرِهِ وَأَظْفَارِهِ**)) وفي راوية: ((**فَلَا يَأْخُذْ مِنْ شَعْرِهِ وَلَا مِنْ أَظْفَارِهِ حَتَّى يُضَحِّي** )) مسلم

Imepokelewa toka kwa Ummu Salamah (رضي الله عنها) kwamba Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: ***((Ukiandama mwezi wa Dhul-Hijjah na ikiwa yuko anayetaka kuchinja basi azuie (asikate) nywele zake na kucha zake))***[16]***.*** Na katika riwaya nyingine: ***((Asikate nywele wala kucha mpaka akimaliza kuchinja))***[17]

Hii ni fadhila na neema kwa Waislamu wasiojaaliwa Hajj kwamba nao watakuwa katika aina ya 'Ihraam'. Ukisahau, mfano ukakata kucha basi endelea tu na niyyah yako mpaka umalize kuchinja.

**vii- Kuhudhuria Swalah ya 'Iyd:**

Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) amewahimiza mpaka wanawake walio katika hedhi na wazee waende kusikiliza khutbah ya Swalaah. Wakati wa Swalaah ukifika, wanawake wenye hedhi wajitenge kando hadi itakapomalizika Swalaah na kisha wajiunge na wenzao kusikiliza khutbah.

---

[15] Ahmad, Ibn Maajah.
[16] Muslim.
[17] Ibn Maajah.

**viii- Siku Za Tashriyq[18]:**

Ni siku ya kumi na moja na kumi na mbili na kumi na tatu ya Dhul-Hijjah yaani baada ya siku ya 'Iyd. Na siku hizi tatu zimeitwa siku za *Tashriyq* kwa sababu watu walikuwa wakikatakata nyama na kuzianika juani. Siku za kuanika (nyama) juani. Na pia siku hizi hujulikana kwa 'siku za *Minaa*'. Ni masiku ya kumdhukuru mno Allaah (سبحانه وتعالى). Haifai kufunga Swawm masiku haya hata kama ni kawaida yake mtu kufunga Swawm za Sunnah kwa sababu amekataza Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) kupitia Hadiyth ya Abu Hurayrah (رضي الله عنه) isemayo:

أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ بَعَثَ عَبْدَ اللَّهِ بْنَ حُذَافَةَ يَطُوفُ فِي مِنًى أَنْ: ((**لَا تَصُومُوا هَذِهِ الْأَيَّامَ فَإِنَّهَا أَيَّامُ أَكْلٍ وَشُرْبٍ وَذِكْرِ اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ**))

Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) alimtuma 'Abdullaah bin Hudhaafah azunguke *Minaa* na atangaze: ((***Msifunge siku hizi, kwani hizi ni siku za kula na kunywa na kumdhukuru Allaah*** **عزَّ وجلَّ**))[19]

[18] Rejea Mlango wa 'Utekelezaji Wa Hajj' Kupata fadhila zake.

[19] Ahmad.